

## **WILAYA YA NYASA KUADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 8/3/2018**

Wilaya ya Nyasa, Mkoa wa Ruvuma itaadhimisha siku ya wanawake duniani itakayofanyika katika Kijiji cha Mbamba Bay, Kata ya Mbamba Bay tarehe 8/3/2018.

Lengo la maadhimisho ni kumuonesha upendo na heshima mwanamke kutokana na mafanikio yake katika nyanja mbalimbali kama vile siasa, kijamii na kiuchumi. Ni siku ambayo wanawake hutambuliwa kutokana na mafanikio yao bila kujali mgawanyiko wa taifa, kabila, lugha, itikadi, kitamaduni, kiuchumi au kisiasa.

Kupitia Umoja wa Mataifa (UN), siku hiyo ilianza kuadhimishwa rasmi mwaka 1975. Miaka miwili baadaye, Desemba mwaka 1977, Baraza Kuu la UN lilipitisha na kutangaza kuadhimisha Siku ya Haki za Wanawake na Amani ya Kimataifa. Tangu kuanza kuadhimishwa kwa siku hiyo ya wanawake duniani, imekuwa na mwelekeo mpya wa kimataifa, kwa ajili ya wanawake katika nchi zote zilizoendelea na zinazoendelea.

Umoja wa Mataifa imekuwa ikisaidia kujenga urithi wa kihistoria wa kimataifa kukubali mikakati na viwango vya mipango na malengo ya kuendeleza hali ya wanawake duniani. Umoja huo na mashirika yake umekuza ushiriki wa wanawake kama washirika sawa na wanaume katika kuleta maendeleo endelevu, amani, usalama, na heshima kwa ajili ya haki za binadamu. Kwa Tanzania maadhimisho hayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka lakini kuanzia mwaka 2005 Serikali ilipitisha uamuzi kuwa, yafanyike kitaifa kila baada ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Nyasa Ndg. Douglas A. Ruambo maadhimisho hayo hutoa fursa kwa Serikali, wananchi, wadau, na wanawake wenyewe kupima utekelezaji wa maazimio, matamko na mikataba ya kimataifa, kikanda na kitaifa inayohusu masuala ya maendeleo ya wanawake na usawa wa jinsia.

“Siku ya wanawake duniani husisitiza kujenga mshikamano wa wanawake wote duniani, kuhamasisha jamii kutafakari kaulimbiu ya maadhimisho hayo kila mwaka; kuelimisha jamii kuhusu jitihada mbalimbali zilizofanywa na Serikali na asasi mbalimbali yakiwemo Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kuwaendeleza wanawake; na kuhamasisha jamii kuhusu utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali ya serikali yenye lengo la kudumisha amani, usawa na maendeleo,” anasema Ruambo.

Wakati Tanzania ikiendelea kupigania haki ya mwanamke kupitia maadhimisho haya, mwaka huu, yataongozwa na kauli mbiu inayosema **“KUELEKEA UCHUMI WA VIWANDA: TUIMARISHE USAWA WA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE VIJIJINI”**.

Maadhimisho haya yataambatana na shughuli za kijamii kama ifuatavyo:-

- 1) Kutoa msaada kwa wazee wa Kambi ya Ngehe, Kata ya Kihagara
- 2) Kushiriki katika upandaji miti kibiashara Kata ya Lipingo
- 3) Kushiriki katika kilele cha maadhimisho tarehe 08/03/2018 katika Kata ya Mbamba-Bay, Kijiji cha Mbamba-Bay kwenye uwanja wa Polisi.